



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA



Kumb. Na. CDC/I 20/2 VOL 1/27

13 /01/ 2021

**YAH: TANGAZO LA UHITAJI WA WATUMISHI WA  
UMMA KUWA NA NAMBA YA UTAMBULISHO WA  
MLIPA KODI (TIN)**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Chemba imepokea barua kumb.na **FA.10/109/01”B”/20** ya tarehe 04 Januari, 2021 toka kwa Katibu Mkuu OR Utumishi ikielekeza Watumishi wa Umma kuwa na namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN Namba)

Kwa tangazo hili Watumishi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba mnatakiwa kuzingatia yafuatayo:

- a. Kuhakikisha kila mtumishi anakuwa na TIN namba ya utambulisho ya mlipa kodi (Taxpayer Identification Number – TIN). Watumishi ambao hawana TIN namba lakini wanakitambulisho cha Taifa au namba za utambulisho wa Taifa (**NIDA**), wanatakiwa kujipatia namba hizo kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa online TIN Registration unaopatikana kupitia tovuti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ambayo ni <https://ots.tra.go.tz>.
- b. watumishi wasio na kitambulisho cha Taifa (NIDA) au namba ya utambulisho wanatakiwa kutembelea Ofisi za TRA ili waweze kupatiwa TIN namba kwa utaratibu uliopo. Aidha, watumishi wenye TIN kwa sasa hawatalazimika kujipatia namba nyingine.

c. Taarifa za TIN namba zinatakiwa kuwasilishwa kama jedwali linavyoonesha hapa chini katika fomati ya "Excel"

### JINA LA TAASISI

| NA | JINA LA MTUMISHI | CHECK NAMBA | TIN NAMBA |
|----|------------------|-------------|-----------|
|    |                  |             |           |
|    |                  |             |           |

**NB:** Waratibu elimu Kata wote, Watendaji wa Kata wote, Waganga wafawidhi wa Vituo vya afya na Zahanati wote, Maafisa ugani wa Kata wote mnatakiwa kuwasilisha taarifa za watumishi mnaowasimamia kwa wakuu wa Idara zenu kabla ama ifikapo tarehe 28 Januari, 2021 bila kukosa.



Dr. Semistatus H. Mashimba  
MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA  
**CHEMBA**

MKURUGENZI MTENDAJI  
WILAYA YA CHEMBA

**Nakala: Mbao za Matangazo Ofisi za Serikali.**